


TCRA: Idadi ya Akaunti za Miamala ya Kifedha Imeongezeka

Na Mwandishi Wetu

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imeweka bayana kwamba idadi ya akaunti zinazotumia huduma za kifedha kupitia simu za mkononi imeendelea kuongezeka katika robo ya pili ya mwaka wa Fedha 2023/2024. Katika taarifa yake iliyochapishwa kwenye tovuti ya Mamlaka hiyo, idadi ya akaunti za miamala ya kifedha imeongezeka kwa asilimia 2.9 kutoka akaunti milioni 51.4 zilizorekodiwa mwezi Septemba mwaka jana hadi kufikia akaunti Milioni 52.9 mwezi Desemba mwaka jana.

Mtoa huduma M-Pesa aliendelea kushika hatamu kwa idadi kubwa zaidi ya akaunti hizo za miamala ya kifedha kwa njia ya simu akiwa na jumla ya waliosajiliwa milioni 20, huku Tigo pesa akifuatia kwa akaunti milioni 16 na Airtel Money akiwa na akaunti milioni 11, na T-Pesa ikiwa na idadi ndogo zaidi ya waliosajiliwa ikiwa na jumla ya akaunti milioni moja laki tatu na sabini mia nne sabini.

Taarifa ya TCRA ilieleza kuwa, akaunti za miamala ya kifedha ziliongezeka kwa kipindi cha robo ya pili ya mwaka wa Fedha kuanzia mwezi oktoba ambapo Mwezi Oktoba kulikuwa na jumla ya akaunti za huduma za kifedha milioni 51.3 mwezi Novemba akaunti milioni 52 na mwezi Desemba akaunti milioni 52.8.



Mgawanyo wa akaunti za kifedha kwa asilimia kwa watoa huduma

TCRA ilieleza kuwa takwimu hizo zinaashiria ushindani mkubwa kwenye soko la Fedha kwa njia ya simu za mkononi huku Tigo Pesa, M-Pesa, na Airtel money zikidhibiti asilimia 90% ya soko la Fedha kwa njia ya simu, M-Pesa ikiwa na asilimia 38% ya udhibiti wa soko hilo.

Takwimu hizi ni muendelezo wa taarifa zinazotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Kila Robo ya Mwaka wa Fedha zikiwasilisha mwenendo wa usimamizi wa sekta ya mawasiliano nchini, ambapo katika eneo la kifedha TCRA hutoa taarifa kuhusu idadi ya miamala na akaunti za kifedha kwa njia ya simu.